**Soma kifungu kifuatacho kwa makini. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Aliyekupa kiti ndiye aliyenipa ___1___ ni ___2___ tuliyoachiwa na watangulizi ___3___. Inatufunza ___4___ na kile tulicho nacho na ___5___ yake tumshukuru Mungu.

Binadamu hawawezi ___6___. Wanaweza ___7___ na vidole ambavyo ni ___8___ na vifupi, vyembamba na vinono. Ukibarikiwa, heri ___9___ na kama ni lazima uongee ___10___ kuwa na hekima. Kamwe usisahau kuwa ulimi hauna ___11___. Mazungumzo ___12___ ya leo yaweza kuwa ndicho ___13___ chake cha ___14___ kesho. Usiwe na ___15___ kwa yeyote. Kumbuka mpanda ngazi hushuka.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ubao | B. kumbi | C. jiwe | D. kibago |
| 2. | A. msemo | B. methali | C. semi | D. ubishi |
| 3. | A. yetu | B. zetu | C. wetu | D. wale |
| 4. | A. tusijiringe | B. tusifurahie | C. tusipende | D. tusiringe |
| 5. | A. baada | B. baadaye | C. badala | D. baada ya |
| 6. | A. kulingana | B. kutoshana | C. kupendana | D. kutoshanishwa |
| 7. | A. kufananishwa | B. kuvananishwa | C. kufanana | D. kukaribiana |
| 8. | A. ndefu | B. refu | C. virefu | D. kirefu |
| 9. | A. ukimye | B. unyamaze | C. unyamase | D. ukakimye |
| 10. | A. unabudi | B. huna budi | C. budini | D. utakuwa na budi |
| 11. | A. mfupa | B. adabu | C. siri | D. meno |
| 12. | A. zako | B. wako | C. yako | D. lako |
| 13. | A. chambo | B. kiama | C. chanzo | D. chano |
| 14. | A. kuchekwa | B. kuchelewa | C. kushekwa | D. kushekelea |
| 15. | A. tharau | B. dharau | C. madharau | D. matharau |



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo.**

16. **Ni nini kinyume cha:**
Kijana alilia kwa huzuni?
A. Msichana alicheka kwa furaha
B. Kijana hakulia kwa huzuni
C. Mvulana alilia kwa huzuni
D. Mzee alicheka kwa furaha

17. Asilimia nukta nane ni:-
A. 80% B. 0.8%
C. 8% D. 8.0%

18. Ng'ombe huyu ni mpole ___________ yule
A. kumliko B. kukuliko
C. kuiliko D. kuliko

19. Kamba, inayoning'inizwa darini kwa kuwekea chungu ili kuhifadhi chakula ni:-
A. Masizi B. Susu
C. Utandu D. Uteo

**Ni nini wingi wa:-**

20. Mkunga alimvua mkunga
A. Mikunga waliwavua wakunga
B. Mikunga alimvua wakunga
C. Wakunga waliwavua mikunga
D. Mikunga waliwavua mikunga

**Tumia kiunganishi kifaacho**


21. Amenunua ndege ______________ gari
A. lau B. kefu
C. bighairi ya D. mithili

22. Yapi si maelezo sahihi kuhusu matumizi ya 'ni'?
A. Hutumiwa pamoja na kihusishi 'ndani ya'
B. Hutumika kama kihusishi
C. Hutumiwa kama kiulizi
D. Hutumika kushurutisha kwa wingi

23. Neno lipi haliambatani na mengine?
A. Tarakilishi B. Darubini
C. Uyoka D. Dohani

24. Wakati baina ya saa sita na saa tisa ni:-
A. alfajiri B. alasiri
C. adhuhuri D. machweo

25. Tambua umbo hili



A. Pembe kali B. Pembe kuu
C. Pembe butu D. Hilali

26. Nomino kiwavijeshi iko katika ngeli gani?
A. I - ZI B. LI - YA
C. KI - VI D. A - WA

27. Utamwitaje mke wa mjomba wako?
A. Halati B. Mkazahau
C. Mkaza ami D. Shangazi

28. Nusu maradufu ni:-
A. $^1/_4$ B. 1
C. $^1/_2$ D. 0

29. Nyambua kitenzi hiki katika kauli ya kutendesha
Lewa:-
A. Levya B. Lewesha
C. Lelewa D. Elewa

30. **Kamilisha methali**
___________ wakunga na uzazi ungalipo
A. Msiwavue
B. Msitukane
C. Msiwapende
D. Uwabeze



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Soma shairi lifuatalo kwa makini kisha ujibu maswali**

Kila uchao twalia, janga lilotukabili,
Twanyong'onyea twalia, na machozi fulifuli
Rabuka twakulilia ,twepushie janga hili,
Jamani tufanye nini, UKIMWI watumaliza!

Ukimwi umeenea, dunia bila kibali,
Afrika na Ulaya, wa'bali wasikubali,
Waja umewatifua , wa aina kila hali,
Jamani tufanye nini, UKIMWI watumaliza!

Nyika ndizo huumia, wapiganapo wawili,
Tusokuwa na hatia, matokeo twakabili,
Wazazi wametufia, tumebaki bila hali,
Jamani tufanye nini, UKIMWI watumaliza!

Mayatima twabakia, tusokuwa na watunza,
Hatuna wa kutukuza, wala nguo kununua,
Kisha tunarandaranda, mapipani kuokota,
Jamani tufanye nini, UKIMWI watumaliza!

Vijana ninauliza, lijibuni swali hili,
Vijana twategemewa, viongozi wa upili,
Ni vipi tutaongoza, msingi wa hii hali,
Jamani tufanye nini, UKIMWI watumaliza.

Tamati nimefikia, ninalia bila hali,
Ukimwi unafagia, yeyote bila kujali,
Watuacha tukilia, pasipo na kutujali,
Jamani tufanye nini, UKIMWI watumaliza!

**31.** Shairi la aina hii huitwaje?

A. UKIMWI

B. Tarbia

C. Tabia

D. Tathlitha

**32.** Katika ubeti wa kwanza, mshororo "Twanyong'onyea twalia, na machozi fulifuli," waitwaje?

A. Mleo

B. Mloto

C. Mwandamizi

D. Mwanzo

**33.** Bainisha mleo katika ubeti wa tano.

A. Vijana ninauliza, lijibuni swali hili,

B. Yeyote bila kujali.

C. Ni vipi tutaongoza, msingi wa hii hali,

D. Ukimwi watumaliza.

**34.** Mwandamizi katika ubeti wa tatu ni:-

A. Wapiganapo wawili

B. Tusokuwa na hatia

C. Hatujapewa

D. Wazazi wametufia, tumebaki bila hali,

**35.** Katika ubeti wa nne, kipande 'wala nguo kununua' chaitwaje?

A. Utao

B. Ukwapi

C. Mwandimizi

D. Mloto



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**36.** Mshairi anaomba nini katika mshororo wa tatu ubeti wa kwanza?

A. Mola awaepushe na janga hili

B. Ukimwi usiwamalize waja wengi

C. Dawa za kupunguza makali

D. Mungu awaepushe na janga la UKIMWI

**37.** Wito upi unaotolewa kwa vijana katika ubeti wa tano?

A. Wanaulizwa swali

B. Vijana wanategemewa kuongoza siku zijazo

C. Vijana hawataongoza

D. Wasome kwa bidii

**38.** Ugonjwa huu unaua akina nani?

A. Wagonjwa B. Kila insi

C. Vijana D. Wazee

**39.** Ni kipi si kisawe cha neno lililopigiwa mstari?

A. Kubali

B. Ruhusa

C. Idhini

D. Ridhaa

**40.** Methali ipi inaafikiana na ubeti wa nne?

A. Usiache mbachao kwa msala upitao

B. Mti mkuu ukigwa wana wa nyuni huyumba

C. Wema hauozi

D. Chovya chovya humaliza buyu la asali

***<u>Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali nambari 41 - 50 .</u>***

Naliaka , binti mdogo mdogo hivi, alitamani kujua Kiswahili . Alishindwa aanzie wapi amalizie wapi. Kwake Kiswahili kilikuwa usiku wa giza. Huo ni usia wa wahenga kwamba jambo usilolijua ni usiku wa giza. Kutokana na waadhi wa penye nia pana njia, alimwendea mwalimu wake wa Kiswahili, Bwana Ketole, kumtaka ushauri .Naam, auguaye huaguliwa. Mwalimu alimpa nasaha, maelekezo na njia mahususi za kujifunza lugha ya Kiswahili.

Mwalimu alimwelekeza jinsi ya kujifunza ufasaha na sarufi kwa kuanzia kwenye ngeli. Baada ya kujifunza ngeli kwa ngeli aliweza kutunga sentensi za neno moja moja. Alipohitimu hatua hiyo, alitunga sentensi fupi fupi na hatimaye sentensi ndefu ndefu za mseto. Maendelezo pia yalikuwa ni matatizo ya aina yake lakini yalitatuliwa kwa kumshauri Naliaka asomesome maandishi ya Kiswahili, hasa Kiswahili aula.

Atafutaye hachoki akichoka keshapata . Naliaka hakuchoka hata baada ya kupata kiasi hicho.Kwani alijua fika kwamba, elimu ni bahari, haina kikomo. Kisha akakumbuka kuwa atangaye sana na jua hujua. Maadili hayo ndiyo yaliyomfikisha Naliaka katika kilele cha upeo wa kufuzu na kufaulu katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Ama kweli, Naliaka kuvuna ni mfano halisi wa kuigwa na kuigika.



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

41. Naliaka alitamani

A. Kujua Kiswahili

B. Kujifunza Kiswahili

C. Kumwuliza mwalimu maswali

D. Lugha ya maswali

42. Awali Naliaka alikuwa na tatizo gani kuu katika hamu yake ya kudurusu Kiswahili?

A. Hakuwa na mwalimu

B. Hakujua mbinu za kuanza kujifunza

C. Aliogopa kumwuliza mwalimu maswali

D. Jambo usilolijua ni usiku wa giza

43. "Auguaye huaguliwa' ni sawa na

A. Mficha uchi hazai

B. Mtaka yote hukosa yote

C. Haba na haba hujaza kibaba

D. Tamaa mbele mauti nyuma

44. 'Kuona neno ndiko kulijua neno' huku hutusaidia katika kuelewa:-

A. Sarufi

B. Sentensi

C. Maendelezo

D. Ngeli

45. Katika kujifunza ufasaha, Naliaka alishauriwa aanze kutalii

A. Sarufi B. Maendelezo

C. Vivumishi D. Ngeli

46. Katika taarifa hii, Naliaka ni mfano wa wanafunzi

A. Wazembe

B. Wenye tamaa

C. Wenye nia

D. Wenye akili

47. Kuelewa kwa mwanafunzi huonekana

A. Anapouliza maswali

B. Anapovumilia

C. Anapopita mtihani

D. Anapojifunza kwa bidii

48. Kauli 'atafutaye hachoki' inarejelea nini?

A. Masomo ya Kiswahili

B. Bidii za kupita mtihani

C. Anayejifunza hakati tamaa

D. Ukitafuta hutachoka

49. Vinavyochangia katika kufaulu kwa mwanafunzi kujifunza si pamoja na:-

A. Subira

B. Stahamala

C. Uvumilivu

D. Faraja

50. Ni muhimu siku zote kuiga

A. Kila kitu

B. Mafunzo yoyote ya Kiswahili

C. Tabia ya wakubwa wetu

D. Matendo mema ya maadili



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com